


# *Masharti ya laa ilaaha illa Allaah*

# *na*

# *mambo yenye kutengua Uislamu*

*Mwandishi:*

**Shaykh Abu ´Abdillaah Muhammad bin Sa´iyd Raslaan**

*Tarjama:*

**Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

1. Utangulizi ........ 3
2. Maana ya laa ilaaha illa Allaah ........ 7
3. Masharti ya laa ilaaha illa Allaah ........ 10
4. Mambo yanayotengua laa ilaaha illa Allaah ........ 25

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

## 1. Utangulizi

Himdi zote zinamstahiki Allaah. Tunamhimidi Yeye, tunamuomba msaada na kumuomba msamaha. Tunajilinda Kwake kutokana na shari ya nafsi zetu na kutokana na uovu wa matendo yetu. Yule mwenye kuongozwa na Allaah, basi hakuna wa kumpoteza, na yule mwenye kupotezwa na Allaah, basi hakuna wa kumwongoza. Ninashuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah na nashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ

**"Enyi mlioamini! Mcheni Allaah kama apasavyo kuogopwa na wala msife isipokuwa nyinyi [mmeshakuwa] ni Waislamu." (03:102)**

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا

**"Enyi watu! Mcheni Mola wenu Ambaye Amekuumbeni kutokana na nafsi moja na Akaumba kutoka humo mke wake na Akaeneza kutoka hao wawili wanaume wengi na wanawake. Na mcheni Allaah Ambaye Kwake mnaombana na jamaa. Hakika Allaah Amekuwa juu yenu *Raqiybaa*, Mwenye kuchunga." (04:01)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ

فَوْزًا عَظِيمًا

**"Enyi mlaomini! Mcheni Allaah na semeni kauli ya kweli [ya sawasawa]. Atakutengenezeeni ‘amali zenu na Kukusameheeni madhambi yenu; na anayemtii Allaah na Mtume Wake, basi kwa yakini amefanikiwa mafaniko adhimu." (33:70-71)**

Amma ba´d:

Hakika maneno ya kweli kabisa ni Qur-aan. Uongofu bora kabisa ni wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mambo maovu kabisa ni ya kuzua. Kila kitakachozushwa ni Bid´ah. Kila Bid´ah ni upotevu. Kila upotevu ni Motoni.

Amma ba´d:

Shaykh-ul-Islaam (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ni jambo limejulikana kwa ulazima katika dini ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Ummah ukakubaliana kwalo ya kwamba asli ya Uislamu na jambo la kwanza ambalo viumbe wanaamrishwa kwalo ni kushuhudia ya kwamba hapana mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah. Kwa hilo ndio kafiri anakuwa muislamu, adui anakuwa kipenzi na damu na mali yake vinakuwa ni venye kulindwa.

Ikiwa hilo amelisema kutoka moyoni mwake, basi ameingia katika imani. Na akilisema kutoka kwenye ulimi wake, pasi na kutoka moyoni mwake, basi kutachukuliwa Uislamu kwa udhahiri pasi na imani kwa ndani.

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaonelea kuwa jambo la kwanza ambalo ni wajibu kwa mja ni kushuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye haki

ya kuabudiwa isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah na kumpwekesha Allaah kwa ´ibaadah. Hoja yao katika hilo ni mambo mengi ikiwa ni pamoja na kauli ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipomwambia Mu´aadh bin Jabal (Radhiya Allaahu ´anh) wakati alipomtuma kwenda Yemen:

**"Hakika wewe unawaendea watu katika Ahl-ul-Kitaab, basi iwe kitu cha kwanza ambacho utawalingania kwacho "hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah."**[1]

Kumpwekesha Allaah kwa Tawhiyd na kujiepusha mbali na shirki ndio jambo la kwanza la wajibu na makalifisho ya wajibu zaidi na faradhi ya kwanza kubwa. Ibn Abiyl-´Izz amesema katika "Sharh-ut-Twahaawiyyah":

"Tambua kuwa Tawhiyd ndio ulinganizi wa kwanza wa Mitume, kituo cha kwanza cha njia na ndio kisimamo cha kwanza anachosimama mtu kuelekea kwa Allaah (´Azza wa Jall). Kwa ajili hii ndio maana ikawa ni sahihi ya kwamba wajibu wa kwanza ambao ni wajibu kwa ambaye ni baleghe na mwenye akili kushuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah."[2]

Amesema tena (Rahimahu Allaah) sehemu nyingine:

"Maimamu wa Salaf wamekubaliana juu ya kwamba kitu cha kwanza anachoamrishwa mja ni Shahaadah mbili."[3]

[1] al-Bukhaariy (1331) na Muslim (19).

[2] (01/59).

[3] Sharh-ut-Twahaawiyyah (01/60).

Neno *laa ilaaha illa Allaah,* hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah ndio neno la Tawhiyd na neno la *Ikhlaasw,* ndio nguzo ya kwanza miongoni mwa nguzo za Uislamu, tawi la kwanza miongoni mwa matawi ya imani, ndio wajibu wa kwanza na muhimu kwa yule ambaye kishabaleghe na ni mwenye akili kama ambavyo vilevile ndio wajibu wake wa mwisho. Hakuna ujuzi wala tendo ambalo ni muhimu zaidi kwa ambaye amekwishabaleghe na ni mwenye akili kuliko hilo.

## 2. Maana ya laa ilaaha illa Allaah

Maana ya *laa ilaaha illa Allaah,* hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah ni kukanusha kustahiki kwa ´ibaadah kwa kila ambaye si Allaah na badala yake kumthibitishia ´ibaadah hiyo Allaah (´Azza wa Jall), peke yake asiyekuwa na mshirika. Hana mshirika katika ´ibaadah Zake kama ambavyo hana mshirika vilevile katika ufalme Wake.

*Laa ilaaha illa Allaah* ina nguzo mbili; ukanushaji na uthibitishaji.

"*Laa ilaah*" ni kukanusha kustahiki kwa ´ibaadah kwa kila asiyekuwa Allaah.

"*Illa Allaah*" unathibitisha kuwa ´ibaadah zote zinamstahiki Allaah peke yake.

Ukanushaji na uthibitishaji ndio Tawhiyd ambayo ilikuja na Mitume na kukateremshwa kwa ajili yake Vitabu. Lengo ilikuwa ni kumthibitishia Allaah uungu peke yake kwa kushuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah, asimwabudu mwingine isipokuwa Yeye, asimtegemei yoyote isipokuwa Yeye, asipendi isipokuwa kwa ajili Yake, asijenge uadui isipokuwa kwa ajili Yake na asifanye ´amali isipokuwa iwe kwa ajili Yake. Hii ndio maana ya neno la ukanushaji na uthibitishaji. Tawhiyd haitimii isipokuwa kwa ukanushaji na uthibitishaji, bi maana kwa kukanusha kustahiki uungu kwa kila asiyekuwa Allaah (Ta´ala), miongoni mwa Mitume hata Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), miongoni mwa Malaika hata Jibriyl, seuze wengine miongoni mwa Mitume na waja wema. Badala yake inatakiwa kumthibitishia uungu Allaah (´Azza wa Jall) peke yake.

Ukanushaji peke yake hautoshelezi na wala uthibitishaji peke yake hautoshelezi. Hayo mawili ni yenye kwenda sambamba. Maana ya *laa ilaaha illa Allaah* ni hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah.

Washirikina wa ki-Quraysh walitambua maana ya *laa ilaaha illa Allaah.* Walisema hali ya kuwa ni wenye kustaajabu kama alivyosema Allaah, Mola wa walimwengu:

أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا ۖ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ

**“Amewafanya miungu [wote] kuwa ni Mungu Mmoja?"[4]**

Vinginevyo ni kwamba wao wanafahamu kuwa Allaah (´Azza wa Jall) ndio Muumbaji Mkubwa na Mwenye kuruzuku Mkarimu. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

**"Na ukiwauliza: “Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi?” bila shaka watasema: “Allaah.”[5]**

Walikuwa ni wenye kujua maana ya *laa ilaaha illa Allaah.* Kwa ajili hiyo ndio maana hawakulisema na wakaendelea kulikataa na hawakulifuata na wakamkadhibisha aliyetumwa nalo (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Mwenye kusema neno hili, hali ya kuwa anatambua maana yake na anajua muqtadhwa yake kukanusha shirki na kuthibitisha Tawhiyd, sambamba na hilo akawa na I´tiqaad yenye maazimio kutokana na yale yaliyobebwa na

[4] 38:05

[5] 31:25

neno hili na akalitendea kazi, basi huyo ndio muislamu wa haki. Na mwenye kufanyia kazi *laa ilaaha illa Allaah* pasi na kuliamini, basi huyo ndio mnafiki wa haki. Na mwenye kufanyia kazi yenye kwenda kinyume nalo katika shirki, basi huyo ndio mshirikina wa haki hata kama atalitamka kwa ulimi wake.

*Laa ilaaha illa Allaah* ni neno kubwa, ndio kishikilio madhubuti, ndio neno la taqwa, ndio neno la *Ikhlaasw*, ndio ambalo kwa ajili yake kumesimamishwa mbingu na ardhi na kukawekwa katika Shari´ah kwa ajili ya kulikamilisha [mambo ya] Sunnah na faradhi. Kwa ajili ya neno hilo ndio kukawekwa Jihaad. Hivyo basi, yule mwenye kulitamka, akalitendea kazi hali ya kuwa ni mkweli, yuko na *Ikhlaasw*, amelikubali na kulipenda, basi Allaah atamwingiza Peponi kutokana na matendo alionayo. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mwenye kushuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah, peke yake asiyekuwa na mshirika, na kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake na kwamba ´Iysaa ni mja na Mtume Wake na ni Neno Lake alompelekea Maryam na roho aloumbwa kutoka Kwake, Pepo ni haki na kwamba Moto pia ni haki, basi Allaah atamwingiza Peponi kutokana na matendo alionayo."**[6]

[6] al-Bukhaariy (3435) na Muslim (28).

## 3. Masharti ya laa ilaaha illa Allaah

Wanachuoni (Rahimahumu Allaah) wamesema kuwa *laa ilaaha illa Allaah* ina masharti saba. *Laa ilaaha illa Allaah* haisihi isipokuwa masharti yake yakikusanyika na mja akayakamilisha. Baadhi yao wameyakusanya katika msemo ufuataao:

*Ujuzi, yakini, Ikhlaasw, ukweli, mapenzi, unyenyekevu, kulikubali*

Shaykh Haafidhw (Rahimahu Allaah) amesema katika "as-Sullam":

*Mwenye kulisema hali ya kuwa anaitakidi maana yake*

*Na akawa ni mwenye kulitenda kazi muqtadhwa yake*

*katika maneno na matendo na akafa ni muumini*

*Atafufuliwa siku ya Qiyaamah hali ya kuwa ni mwenye kuokoka na muumini*

*Maana yake imetolewa dalili na yakini na ikaongoza kuelekea kwayo*

*ya kwamba hakuna mungu anayeabudiwa kwa haki*

*Isipokuwa Allaah, Mmoja, Aliyepwekeka*

*kwa kuumba, kutoa riziki na kuendesha mambo*

*Ametakasika na washirika na wenza*

*Imefungamanishwa na masharti saba*

*Yamethibiti kwa haki katika maandiko ya Wahyi*

*Mwenye kuitamka hanufaiki kwayo*

*isipokuwa kwa kutimiza masharti hayo*

*ujuzi, yakini na kukubali*

*na kunyenyekea, yajue ninayoyasema*

*ukweli, Ikhlaasw na kupenda*

*Allaah akuwafikishe kwa yale anayoyapenda*

Kuhusiana na ufafanuzi wa masharti hayo:

Ya kwanza: Ujuzi. Kuwa na ujuzi wa *laa ilaaha illa Allaah* kwa maana ya ukanushaji na uthibitishaji na kuwa na ujuzi wa matendo inayoyalazimu.

Mja akijua kuwa Allaah (´Azza wa Jall) ndiye mwenye kuabudiwa peke yake, hali ya kuwa hana mshirika na kuwa ´ibaadah kwa wengine ni batili na akafanyia kazi muqtadhwa wa ujuzi huo. Basi huyo atakuwa ni mjuzi wa maana ya *laa ilaaha illa Allaah.*

Kinyume cha ujuzi ni ujinga kwa njia ya kwamba mtu akawa hajui uwajibu wa kumpwekeshea Allaah ´ibaadah. Bali yeye akawa anaonelea kuwa inajuzu kumuabudu mwingine pamoja na Allaah. Allaah (Ta´ala) amesema:

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ

**"Basi jua ya kwamba hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah."[7]**

Sharti ya kwanza ya *laa ilaaha illa Allaah* ni kujua maana yake kwa kukanusha na kuthibitisha na matendo inayoyalazimu. Anatakiwa awe na ujuzi usiokuwa na ujinga. Amesema (Ta´ala):

[7] 47:19

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ

**"Basi jua ya kwamba hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah."[8]**

وَلَا يَمْلِكُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الشَّفَاعَةَ إِلَّا مَن شَهِدَ بِالْحَقِّ

**"Na wala wale wanaowaomba badala Yake hawana [uwezo] wa kumiliki uombezi isipokuwa yule aliyeshuhudia kwa haki..."**

bi maana wameshuhudia *laa ilaaha illa Allaah.*

وَهُمْ يَعْلَمُونَ

**"... nao wanajua."[9]**

wanajua kwa mioyo yao maana ya yaliyotamkwa kwa ndimi zao. ´Uthmaan bin ´Affaan (Radhiya Allaahu ´anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mwenye kufa hali ya kuwa anajua kuwa hapana mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah ataingia Peponi."[10]**

Ya pili: Yakini. Atamke Shahaadah kwa yakini ya azima hali ya kuwa moyo wake umetulia juu yake pasi na kuwa na shaka yoyote ile na huku awe ni mwenye kuitakidi usahihi wa yale anayoyasema juu ya kustahiki uungu

---

[8] 47:19

[9] 43:86

[10] Muslim (26).

kwa Allaah (Ta´ala) na kubatilika uungu kwa asiyekuwa Yeye na kwamba haijuzu kumfanyia aina yoyote ya ´ibaadah asiyekuwa Allaah. Akiwa na shaka katika Shahaadah yake au akanyamaza na asiseme kitu juu ya ubatili wa kumfanyia ´ibaadah asiyekuwa Allaah, kwa mfano aseme kuwa yeye anayakinisha uungu wa Allaah lakini ana mashaka juu ya ubatilikaji wa uungu kwa asiyekuwa Allaah, Shahaadah yake inabatilika na haitomfaa. Amesema (Ta´ala) akiwasifu waumini:

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ

**"Na ambao huamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako na ni wenye yakini na Aakhirah."[11]**

Akawasifu tena waumini kwa kusema:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا

**"Hakika Waumini ni wale waliomwamini Allaah na Mtume Wake kisha wakawa si wenye shaka."[12]**

Yakini yenye azima ni ile ambayo moyo umetulia juu yake na haina shaka yoyote na huku anaitakidi usahihi wa anayoyasema kwa ulimi wake juu ya kustahiki uungu kwa Allaah (´Azza wa Jall) na kubatilika uungu kwa asiyekuwa Yeye na kwamba haijuzu kumfanyia yoyote asiyekuwa Allaah katika aina za uungu na ´ibaadah. Muslim amepokea katika "as-Swahiyh" yake kwa mlolongo wa wapokezi wake kupitia kwa Abu Hurayrah

[11] 02:04

[12] 49:15

(Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Ninashuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba mimi ni Mtume wa Allaah, Allaah hakutani na mja akiwa na maneno hayo mawili pasi na kuwa na shaka kwayo, isipokuwa atamwingiza Peponi."**[13]

Ni lazima kuwepo yakini juu ya *laa ilaaha illa Allaah.*

Kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mwenye kukutana na mimi nyuma ya bustani hili akiwa ni mwenye kushuhudia kuwa hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah na moyo wake ni wenye yakini kwayo, basi ninambashiria Pepo."**[14]

Hii ndio sharti ya pili ya *laa ilaaha illa Allaah.* Ya kwanza ni ujuzi wa kujua ya kwamba hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah na kwamba ni wajibu kumpwekesha Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) kwa ´ibaadah dhahiri na kwa ndani. Ya pili awe na yakini ndani ya moyo juu ya jambo hili. Amesema (Ta´ala):

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

[13] Muslim (27).

[14] Muslim (31).

**"Hakika Waumini ni wale waliomwamini Allaah na Mtume Wake kisha wakawa si wenye shaka na wakafanya jihaad kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Allaah. Hao ndio wakweli."[15]**

Katika ukweli wa kumuamini kwao Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameshurutisha wasiwe ni wenye mashaka. Kuhusiana na yule mwenye kutilia shaka ni katika wanafiki ambao Allaah amesema juu yao:

إِنَّمَا يَسْتَأْذِنُكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَارْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِي رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُونَ

**"Hakika wanaokuomba ruhusa [ya kubakia nyuma] ni wale ambao hawamwamini Allaah na Siku ya Mwisho, na nyoyo zao zina shaka, basi wao katika shaka zao wanasitasita."[16]**

Hana imani yule mwenye kuitamka huku akiwa na mashaka na wasiwasi, hata kama ataisema kwa idadi ya pumzi zake, hata kama ataisema kwa sauti ya juu mpaka watu wote waisikie. Imekuja katika Hadiyth:

**"Ninashuhudia ya kwamba hakuna mungu isipokuwa Allaah na kwamba mimi ni Mtume wa Allaah, Allaah hakutani na mja akiwa na maneno hayo mawili hali ya kuwa si mwenye shaka kwayo, isipokuwa ataingia Peponi."**

Kusema mwenye kuitamka aingie Peponi imeshurutishwa moyo wake uwe na uyakinifu pasi na kuwa na shaka. Kukikosekana sharti kunakosekana kilichoshurutishwa kwa ajili yake. Haingii Peponi isipokuwa yule ambaye moyo wake una uyakinifu.

---

[15] 49:15

[16] 09:45

Ya tatu: Kukubali. Anatakiwa kukubali kila ambacho kinahitajia neno hili kwa moyo na ulimi wake. Asadikishe maelezo na kuamini kila kilichokuja kutoka kwa Allaah kupitia njia ya Mtume mteuliwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ayakubali yote hayo na asirudishe chochote na asiyavamie maandiko kwa Ta´wiyl mbovu na upotoshaji ambao Allaah amekataza.

Kinyume cha kukubali ni kurudisha. Kuko ambao wanajua maana ya Shahaadah na wanayakinisha yanayotolewa dalili nayo. Anatekeleza sharti ya kwanza na ya pili lakini hata hivyo anairudisha kwa kiburi na hasadi. Hii ndio hali ya mayahudi na manaswara. Allaah (Ta´ala) amesema:

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ أَبْنَاءَهُمْ ۖ وَإِنَّ فَرِيقًا مِّنْهُمْ لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

**"Wale Tulioewapa Kitabu wanatambua kama wanavyotambua watoto; na hakika kundi miongoni mwao wanaficha haki na hali wao wanajua."**[17]

Kunaingia katika neno kukataa kwa kuvunja sharti ya tatu miongoni mwa masharti ya *laa ilaaha illa Allaah* yule mwenye kufanya upinzani na baadhi ya maandiko ya Kishari´ah au baadhi ya adhabu za Kishari´ah na akayarudisha. Kwa mfano wale wenye kupingana na adhabu ya mwizi, wenye kupingana na adhabu ya zinaa na wale wenye kupingana na suala la kuoa wake wengi. Yote haya yanaingia katika neno kukataa na kutokubali *laa ilaaha illa Allaah.*

Ya nne: Kunyenyekea kunakopingana na kuacha. Anyenyekee kwa yale yenye kutolewa dalili na neno la *Ikhlaasw.* Pengine tofauti kati ya kunyenyekea na kukubali ni kuwa kukubali ni kudhihirisha kusihi maana yake kwa maneno kwa njia ya kwamba anayakubali na kuonesha kwa uinje

[17] 02:146

kuwa anayatamka kwa ulimi. Ama kunyenyekea ni kufuata kwa matendo. Yote mawili yanalazimisha kufuata. Kunyenyekea ni kujisalimisha na kutopingana na kitu katika hukumu za Allaah. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ

**“Na rejeeni [kutubu] kwa Mola wenu na jisalimisheni Kwake."[18]**

Vilevile kunyenyekea yale yaliyokuja na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kuyaridhia na kuyafanyia kazi bila ya kupingana nayo, kuzidisha wala kupunguza. Amesema (Ta´ala):

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

**"Basi Naapa kwa Mola wako, hawatoamini mpaka wakufanye wewe ni hakimu [mwamuzi] katika yale wanayozozana baina yao, kisha wasipate katika nyoyo zao karaha katika yale uliyohukumu na wajisalimishe, kwa kujisalimisha [kikamilifu]."[19]**

Mtu akijua maana ya *laa ilaaha illa Allaah* basi atakuwa ametekeleza sharti ya kwanza. Akiiyakinisha atakuwa ametekeleza sharti ya pili. Akiikubali atakuwa ametekeleza sharti ya tatu. Lakini pamoja na hivyo asiponyenyekea na asijisalimishe nayo na wala asifanye muqtadhwa wa aliyojifunza, basi hilo halitomfaa kitu.

Moja katika kutokunyenyekea ni kuacha kuhukumiwa kwa Shari´ah ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) na badala yake kuhukumiwa kwa sheria za binaadamu.

[18] 39:54

[19] 04:65

Ya tano: Ukweli. Mtu kuwa na ukweli na Allaah kwa njia ya kwamba awe ni mkweli katika imani yake na ´Aqiydah yake. Pindi atapokuwa hivyo basi hapo ndipo atakuwa mkweli juu ya yale yaliyokuja katika Qur-aan na Sunnah.

Ukweli ndio msingi wa maneno. Miongoni mwa ukweli ni awe na ukweli katika ulinganizi wake na atumie juhudi katika kumtii Allaah na kuihifadhi mipaka ya Allaah. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ

**"Enyi mlioamini! Mcheni Allaah na kuweni pamoja na wakweli."[20]**

Sharti ya ukweli imethibiti katika Hadiyth ambayo ni Swahiyh kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mwenye kusema *laa ilaaha illa Allaah* mkweli kwayo, basi ataingia Peponi."[21]**

Ni Hadiyth Swahiyh iliyopokelewa na Imaam Ahmad.

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Hakuna yeyote mwenye kushuhudia kuwa hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah hali ya kuwa ni mkweli kutoka katika moyo wake isipokuwa Allaah atamharamishia Moto."[22]**

[20] 09:119

[21] Ahmad (19100) na ni Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaamiy´" (35).

[22] al-Bukhaariy (128) na Muslim (32).

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim kupitia katika upokezi wa Mu´aadh.

Kinyume cha ukweli ni uongo. Mtu akiwa ni muongo katika imani yake basi hazingatiwi kuwa ni muumini. Bali ni mnafiki hata kama atatamka Shahaaadah kwa ulimi wake. Hali ya mnafiki huyu ni mbaya zaidi kuliko hali ya kafiri ambaye anadhihirisha kufuru. Akitamka Shahaadah kwa ulimi wake na akakanusha yanayotolewa dalili nayo kwa moyo wake, basi Shahaadah hii haitomwokoa. Badala yake anaingia katika idadi ya wanafiki. Amesema (Ta´ala):

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ

**"Na miongoni mwa watu wako wasemao: ″Tumemuamini Allaah na Siku ya Mwisho″ hali ya kuwa si wenye kuamini."[23]**

Miongoni mwa mambo ambayo yanapingana na ukweli katika Shahaadah ni kukadhibisha yale aliyokuja nayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) au kukadhibisha baadhi ya aliyokuja nayo (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah (Ta´ala) ametuamrisha kumtii na kumfuata (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na akafanya hilo ni kwenda sambamba na kumtii Yeye. Amesema (Subhaanah):

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ

**"Na mtiini Allaah na mtiini Mtume."[24]**

Sharti ya tano miongoni mwa masharti ya *laa ilaaha illa Allaah* ni ukweli.

[23] 02:08

[24] 64:12

Ya sita: Ikhlaasw. Ikhlaasw ni mtu kutakasa kitendo chake kwa nia njema kutokana na uchafu wote ikiwa ni pamoja na uchafu wa shirki na uchafu mwingine. Hilo linakuwa kwa maneno yake yote yanayomtoka na matendo yote anayofanya awe anafanya hivo kwa ajili ya Allaah na kutafuta radhi za Allaah. Kusiwe katika mambo hayo uchafu wa kutaka kujionyesha au kusikika, maslahi, makusudio ya kibinafsi au matamanio ya dhahiri au yaliyojificha. Amesema (Ta´ala):

أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ

**"Tanabahi! Ni ya Alllaah Pekee Dini iliyotakasika."25**

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

**"Na hawakuamrishwa [chochote kile] isipokuwa wamwabudu Allaah kwa kumtakasia Yeye Dini."[26]**

Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Mtu ambaye ni aula zaidi kupata uombezi wangu siku ya Qiyaamah ni yule aliyesema *laa ilaaha illa Allaah* akiwa na *Ikhlaasw* kutoka katika moyo wake."[27]**

Ni lazima ipatikane sharti ya *Ikhlaasw.*

[25] 39:03

[26] 98:05

[27] al-Bukhaariy (99).

Katika "as-Swahiyh" al-Bukhaariy na Muslim kupitia Hadiyth ya ´Itbaan (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Allaah ameharamisha Moto kwa yule mwenye kusema *laa ilaaha illa Allaah* akikusudia kwa kusema hivo Uso wa Allaah."[28]**

Allaah (Subhaanah) amesema hali ya kuwa ni mwenye kubatilisha matendo ya watu wa shirki:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا

**"Hakika Allaah Hasamehi kushirikishwa; lakini Anasamehe yasiyokuwa hayo kwa Amtakae. Na yeyote atakayemshirikisha Allaah basi kwa yakini amebuni dhambi kuu."[29]**

Ya saba: Kupenda neno hili la *laa ilaaha illa Allaah* na yale yanayotolewa dalili nalo na masharti yanayopelekea katika *laa ilaaha illa Allaah,* hii ndio sharti ya saba. Sharti ya kupenda. Ina maana ya kwamba anampenda Allaah na kumpenda Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Atangulize mapenzi ya *laa ilaaha illa Allaah* juu ya kila mapenzi. Vilevile asimamishe masharti ya mapenzi na malazimisho yake. Anapaswa kumpenda Allaah mapenzi yenye kuambatana na matukuzo na uadhimisho, khofu na matarajio. Anatakiwa kupenda kile anachopenda Allaah miongoni mwa sehemu kama Makkah, al-Madiynah na Misikiti kwa jumla. Apende zile zama anazozipenda Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) kama Ramadhaan, siku kumi za Dhul-Hijjah na nyenginezo. Awapende wale watu anaowapenda Allaah katika Manabii, Mitume, wakweli, mashahidi

[28] al-Bukhaariy (425) na Muslim (33).

[29] 04:48

na waja wema. Vilevile anatakiwa kupenda matendo anayoyapenda Allaah kama swalah, zakaah, swawm na hajj. Anatakiwa kupenda maneno yanayopendwa Allaah kama Dhikr na kusoma Qur-aan.

Katika kumpenda Allaah ni pamoja vilevile na kutanguliza yale anayoyapenda Allaah juu ya yale yanayopendwa na kutamaniwa na nafsi. Kwa sababu Pepo imezungukwa na matamanio na Moto umezungukwa na vitu vyenye kuchukiza.

Miongoni mwa kumpenda Allaah anatakiwa vilevile kumchukia yule anayemchukia Allaah. Vinginevyo atakuwa si mkweli katika kumpenda kwake Allaah. Kwa sababu haingii akilini akawa ni mwenye kumpenda Allaah (´Azza wa Jall) na wakati huo huo akampenda adui wa Allaah, Mola wa walimwengu. Hivyo awachukie makafiri, kuwabughudhi, kuwa na uadui nao na achukie kufuru, ufuska na uasi. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَن يَرْتَدَّ مِنكُمْ عَن دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ

**"Enyi mlioamini! Yeyote atakayeritadi miongoni mwenu kutoka Dini yake, basi Allaah Ataleta watu [badala yao] Atakaowapenda nao watampenda; wanyenyekevu kwa Waumini, wenye nguvu juu ya makafiri; wanafanya jihaad katika njia ya Allaah na wala hawakhofu lawama ya [yeyote] anayelaumu."**[30]

Kumpenda kwao Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) hakutowafaa kitu kwa kuwa wamempenda mwingine pamoja na Allaah na hivyo Allaah akawa ni mwenye kuyabatilisha matendo yao na akawaingiza Motoni humo watadumu milele:

[30] 05:54

وَمَا هُم بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ

**"Na wala hawatokuwa wenye kutoka Motoni."**[31]

Miongoni mwa mambo yanayopingana na kupenda ni kumchukia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Miongoni mwa mambo yanayopingana na kupenda ni kuwapenda maadui wa Allaah katika mayahudi, manaswara na washirikina wengine.

Miongoni mwa mambo vilevile yanayopingana na kupenda ni kuwachukia mawalii wa Allaah ambao ni waumini.

Vilevile katika mambo yanayopingana na ukamilifu wa kupenda ni kufanya maasi na madhambi.

Haya ndio masharti ya *laa ilaaha illa Allaah.* Yule asiyeyatekeleza na kutoyatimiza kwa sura yake stahiki, basi *laa ilaaha illa Allaah* haitomfaa.

*Laa ilaaha illa Allaah* ni ufunguo wa Pepo, hili ni jambo sahihi. Lakini hata hivyo hakuna ufunguo wowote isipokuwa una meno. Ukija na ufunguo ulio na meno utafunguliwa na usipokuwa na ufunguo usiokuwa na meno basi hutofunguliwa na ufunguo wako hautokufaa kitu.

*Laa ilaaha illa Allaah* ni sababu ya kuingia Peponi na kuokoka na Moto na jambo linalopelekea katika hilo. Lakini hata hivyo ni lazima kutimie masharti yake na kusiwepo kikwazo chake. Muqtadhwa wake unaweza kuingiwa na kasoro kwa kukosekana sharti miongoni mwa masharti yake au kwa kupatikana kikwazo miongoni mwa vikwazo vyake. Kwa ajili hii kulisemwa kuambiwa al-Hasan:

[31] 02:167

"Watu wanasema kuwa mwenye kusema *laa ilaaha illa Allaah* ataingia Peponi."

Akasema: "Mwenye kusema *laa ilaaha illa Allaah* akaitekelezea haki na faradhi zake ataingia Peponi."

Wahb bin Munabbih alisema kumwambia aliyeuliza: "Je, *laa ilaaha illa Allaah* si ni ufunguo wa Pepo"? Akajibu kwa kusema:

"Ndio, lakini hata hivyo hakuna ufunguo wowote isipokuwa una meno. Ukija na ufunguo wenye meno utafunguliwa na la sivyo hufunguliwi."

Haya ndio masharti ya *laa ilaaha illa Allaah* ambayo hayamfai mja isipokuwa pale atapoyakamilisha na kufanyia kazi muqtadhwa wake.

Hivyo basi unatakiwa kuyajua na kuyahakikisha na kuyatenda kazi ili usije kutumbukia kwenye kitu kinachovunja *laa ilaaha illa Allaah*. Allaah amewajibisha kwa viumbe vyote kuingia katika Uislamu na kushikamana nao na kutahadhari na mambo yanayoenda kinyume nao. Allaah amemtuma Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ili kulingania katika hilo. Allaah (´Azza wa Jall) akaeleza kuwa mwenye kumfuata ameongoka, na yule mwenye kumpa mgongo basi amepotea. Katika Aayah nyingi ametahadharisha sababu za kuritadi na aina mbali mbali za shirki na kufuru.

## 4. Mambo yanayotengua laa ilaaha illa Allaah

Wanachuoni (Rahimahumu Allaah) wametaja katika mlango: "Hukumu ya mwenye kuritadi" ya kwamba muislamu anaweza kuritadi kutoka katika dini yake - tunamuomba Allaah afya - kwa aina mbali mbali miongoni mwa aina zinazotengua Uislamu ambazo zinahalalisha damu na mali yake. Na hivyo anakuwa ni mwenye kutoka katika Uislamu.

Miongoni mwa vitu vinavyotengui Uislamu vya khatari sana na vinavyotokea mara nyingi ni vitu kumi:

Cha kwanza: Kumshirikisha Allaah. Amesema (Subhaanah):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا

**"Hakika Allaah Hasamehi kushirikishwa; lakini Anasamehe yasiyokuwa hayo kwa Amtakae. Na yeyote atakayemshirikisha Allaah basi kwa yakini amebuni dhambi kuu."[32]**

إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ

**"Hakika mwenye kumshirikisha Allaah bila shaka Allaah Atamharamishia Jannah, na makazi yake yatakuwa ni Motoni - na madhalimu hawatopata mwenye kunusuru yeyote."[33]**

Miongoni mwa mambo hayo ambayo yanavunja Uislamu na yanamtoa mtu katika Uislamu ni pamoja na kuwaomba maiti, kuwataka msaada,

[32] 04:48

[33] 05:72

kuwawekea nadhiri na kuchinja kwa ajili yao. Yote haya ni miongoni mwa mambo makubwa yanayotengua Uislamu.

Cha pili: Mwenye kuweka baina yake na baina ya Allaah mkati na kati akawa anamuomba, anawataka uombezi na kumtegemea. Huyu amekufuru kwa maafikiano. Amesema (Subhaanah):

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ ۖ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِن شِرْكٍ وَمَا لَهُ مِنْهُم مِّن ظَهِيرٍ وَلَا تَنفَعُ الشَّفَاعَةُ عِندَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ

**"Sema: "Ombeni wale mnaodai [kuwa ni miungu] badala ya Allaah, hawamiliki uzito wa atomu [au sisimizi] mbinguni wala ardhini, na wala [wao] hawana humo ushirika [Naye], na wala [Allaah] Hana msaidizi miongoni mwao." Na wala hautofaa uombezi mbele Yake isipokuwa kwa yule Aliyempa idhini."[34]**

وَلَا تَدْعُ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ۖ فَإِن فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذًا مِّنَ الظَّالِمِينَ وَإِن يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَادَّ لِفَضْلِهِ ۚ يُصِيبُ بِهِ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۚ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

**"Na usiombe badala ya Allaah asiyekufaa [ukimwabudu] na wala asiyekudhuru [usipomwabudu]. Na ukifanya [hivyo], basi hakika utakuwa miongoni mwa madhalimu." Na Allaah Akikugusisha dhara, basi hakuna wa kuiondosha isipokuwa Yeye. Na Akikutakia kheri, basi hakuna wa kurudisha fadhila Zake, Anasababisha kumfikia kwayo Amtakaye katika waja Wake. Naye ni *Al-Ghafuwrur-Rahiym*, Mwingi wa kusamehe - Mwenye kurehemu."[35]**

[34] 34:22-23

[35] 10:106-107

Mwenye kuweka kati yake yeye na kati ya Allaah wakati na kati ambapo akawa anawaomba, anawataka uombezi, anawategemea na anawaogopa woga wa siri basi amekufuru kwa maafikiano ya wanachuoni wa Kiislamu.

Cha tatu: Asiyewakufurisha washirikina, akatilia shaka kukufuru kwao au akaonelea kuwa madhehebu yao ni sahihi anakufuru. Amesema (Subhaanah):

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَآءُ مِنكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحْدَهُ

**"Kwa yakini mna kigezo kizuri kwa Ibraahiym na wale walio pamoja naye, walipowaambia watu wao: "Hakika sisi tumejitenga mbali nanyi na yale [yote] mnayoyaabudu badala ya Allaah, tunakukanusheni, na umedhihirika baina yetu na baina yenu uadui na bughudha milele mpaka mumuamini Allaah Pekee."[36]**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ ۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiwachukuwe Mayahudi na Manaswara kuwa ni marafiki - wao kwa wao ni marafiki. Na yeyote atakayewafanya marafiki wao; basi hakika yeye ni miongoni mwao. Hakika Allaah Haongoi watu madhalimu."[37]**

**Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam): "Mwenye kusema *hapana mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah* na**

[36] 60:04

[37] 05:51

**akakufuru vyenye kuabudiwa badala ya Allaah, basi mali na damu yake ni haramu na hesabu yake iko kwa Allaah."**[38]

Ameipokea Muslim.

Cha nne: Mwenye kuamini kuwa kuna uongofu bora usiokuwa wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) au hukumu ambayo ni bora kuliko hukumu yake. Mfano wa watu hawa ni wale wenye kufadhilisha hukumu ya mashaytwaan juu ya hukumu yake, hawa ni makafiri.

Vilevile yule mwenye kuamini kuwa sheria za binaadamu ambazo binaadamu wanatunga ni bora kuliko Shari´ah ya Kiislamu, akaamini kuwa ziko sawa sawa au akaamini kuwa inajuzu kuhukumiwa kwazo, hata kama ataamini kuwa bora ni kuhukumiwa kwa Shari´ah, akaamini kuwa Shari´ah haeidani na kutumiwa katika karne ya ishirini, Shari´ah ndio sababu ya waislamu kuwa nyuma au kwamba mafungamano ya Uislamu yamekomeka kati ya mja na Mola Wake Msikitini peke yake na kuwa Uislamu hauingilii masuala mengine ya kimaisha.

Kunaingia katika hilo pia yule mwenye kuonelea kuwa kutekeleza hukumu ya Allaah kukata mkono wa mwizi, kumpiga mawe mzinifu muoaji/muolewaji na kwamba jambo hili haliendani na wakati wa sasa na akasema kuwa ni unyama ambao watu wanatakiwa kuacha.

Kunaingia katika hilo pia kila yule mwenye kuamini kuwa inajuzu kuhukumu kinyume na Shari´ah ya Allaah katika mambo ya mu´amala, adhabu za Kishari´ah au mambo mengine hata kama hatoamini kuwa hukumu hiyo ni bora kuliko Shari´ah. Kwa sababu kwa kufanya hivo atakuwa amehalalisha kitu alichoharamisha Allaah miongoni mwa mambo

[38] Muslim (23).

ambayo yanajulikana fika katika dini mfano wa zinaa, pombe, ribaa na hukumu kinyume na Shari´ah. Mwenye kufanya kitu katika hayo ni kafiri kwa maafikiano ya waislamu.

Kuhusiana na kuhukumu kinyume na aliyoteremsha Allaah kutokana na matamanio ndani ya nafsi, kutokujua yale aliyoteremsha Allaah na wakati huo huo anaamini kuwa hukumu ya Allaah ndio haki na ndio wajibu, huyu ametenda dhambi kubwa miongoni mwa madhambi makubwa na amefanya kufuru ndogo.

Cha tano: Mwenye kuchukia kitu miongoni mwa mambo aliyokuja nayo Mtume hata kama atakifanya kitu hicho. Akikifanya na huku anakichukia, basi huyo ni kafiri. Amesema (Ta´ala):

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ

**"Hivyo kwa kuwa wao wameyachukia yale Aliyoyateremsha Allaah, basi Ameziporomosha ‘amali zao."**[39]

Cha sita: Mwenye kufanyia mzaha kitu miongoni mwa mambo ya dini ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), thawabu au adhabu anakufuru. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

**"Na ukiwauliza bila shaka watasema: “Hakika tulikuwa tunaporoja na tunacheza.” Sema: Je, mlikuwa mnamfanyia istihizai Allaah na *Aayaat* Zake na Mtume Wake?” Msitoe udhuru.**

[39] 47:09

**Mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu."[40]**

Cha saba: Uchawi. Ni kitu kikubwa kinachovunja Uislamu. Miongoni mwa uchawi ni pamoja na *as-Swarf* ambapo ni kitendo cha uchawi kinachofanywa kwa lengo la kumzuia mtu na kufanya jambo la kheri na kumkimbiza na mke wake.

Vilevile kuna *al-´Atwf* ambacho ni kitendo cha uchawi kinachofanywa kwa lengo la mume aweze kumpenda mke wake na mengineyo kwa kutumia njia ya uchawi.

Mwenye kufanya haya au akayaridhia anakufuru. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ

**"Na hawamfundishi yeyote mpaka wamueleze: “Hakika sisi ni mtihani, basi usikufuru."[41]**

Cha nane: Kuwapa nguvu washirikina na kuwasaidia dhidi ya waislamu. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ ۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**"Enyi mlioamini! Msiwachukuwe Mayahudi na Manaswara kuwa ni marafiki - wao kwa wao ni marafiki. Na yeyote atakayewafanya**

[40] 09:65-66

[41] 02:102

**marafiki wao; basi hakika yeye ni miongoni mwao. Hakika Allaah Haongoi watu madhalimu."[42]**

Cha tisa: Mwenye kuamini kuwa baadhi ya watu wanaweza kutoka katika Shari´ah ya Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwenye kuamini hivo ni kafiri. Amesema (Ta´ala):

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

**"Na yeyote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitokubaliwa kwake; naye katika Aakhirah atakuwa miongoni mwa waliokhasirika."[43]**

Hakuna dini ya haki yoyote isipokuwa ya Muhammad tu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Cha kumi: Kupuuzia dini ya Allaah kwa njia ya kwamba hajifunzi nayo na wala haifanyii kazi. Dalili ni Kauli Yake (Ta´ala):

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا ۚ إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ

**"Na nani dhalimu zaidi kuliko yule anayekumbushwa *Aayaat* za Mola wake, kisha akakengeuka nazo [kuzipuuza]? Hakika Sisi Tutawalipiza wahalifu."[44]**

Hakuna tofauti katika mambo haya yanayotengua Uislamu baina ya mwenye kufanya mzaha na mwenye kukusudia kweli, mwenye kuogopa na mwenye kufanya mchezo. Isipokuwa tu aliyetenzwa nguvu, huyu ana

[42] 05:51

[43] 03:85

[44] 32:22

hukumu yake. Ama kuhusiana na mwenye kufanya mzaha kwa kitu katika hayo, kucheza na dini ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala), ni kitu kinachomtoa katika Uislamu na kuvunja Uislamu wake:

وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ ۚ إِن نَّعْفُ عَن طَائِفَةٍ مِّنكُمْ نُعَذِّبْ طَائِفَةً بِأَنَّهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ

**65. Na ukiwauliza bila shaka watasema: "Hakika tulikuwa tunaporoja na tunacheza." Sema: Je, mlikuwa mnamfanyia istihizai Allaah na *Aayaat* Zake na Mtume Wake?" Msitoe udhuru. Mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu. Tukilisamehe kundi miongoni mwenu, Tutaliadhibu kundi [jingine], kwa kuwa wao walikuwa wahalifu."**[45]

Yote haya ni miongoni mwa mambo ya khatari na yanayotokea sana. Inatakikana kwa muislamu atahadhari nayo, ayaogope kwenye moyo wake, aombe kinga kwa Allaah kwa yale yanayowajibisha hayo na khasira za Allaah na adhabu Yake kali. Badala yake ajitahidi kuhakikisha *laa ilaaha illa Allaah* na ajue mambo yanayotengua Uislamu ili aweze kutahadhari nayo na atahadharishe nayo.

Waislamu watahadhari kumpachika mtu kwa dhati yake hukumu hizi za kijumla pasi na kutimia masharti, kutokuwepo vizuizi na kusimamisha hoja. Asiwakufurishe waislamu bila ya haki na hivyo akawa ni mwenye kuingia katika kauli ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mwenye kumwambia ndugu yake "ee kafiri", itakuwa ni kama alivyosema la sivyo itamrejelea mwenyewe."**

[45] 09:65-66

Waislamu wanatakiwa kujua kuwa kumkufurisha muislamu pasina haki ni jambo kubwa zaidi ya kumuua. Enyi watu! Mcheni Allaah.

Tunamuomba Allaah, Mola wa walimwengu atuthibitishe juu ya dini Yake yenye imani safi mpaka hapo tutapokutana na Uso Wake Mtukufu.

Ee Allaah, Mola wa walimwengu! Tuthibitishe katika Uislamu na tuwe ni wenye kushikamana nao mpaka hapo tutapokutana na Uso Wako Mtukufu.

Swalah na salaam zimwendee Mtume Wetu Muhammad na baba zake Ibraahiym na Ismaa´iyl na Mitume na wajumbe waliosalia, ahli zake na Maswahabah zake wote.